

## **MKATABA WA UCHANGIAJI WA GHARAMA ZA MATUMIZI YA JENGO**

Mkataba huu utanza kutumika rasmi tarehe 1 August 2023.

### **KATI YA**

**AFISA MADINI MKAZI WA MBEYA S.L.P. 760, MBEYA** ambaye atajulikana kama **"mpangishaji"** kwa upande mmoja.

### **NA**

**ELDORADO HOLDINGS TZ LTD S.L.P 260, MBEYA** , ambaye atajulikana kama **"mpangaji"** kwa upande mwingine.

**AMBAPO MPANGISHAJI** ni mmiliki wa jengo la ghorofa tano lililoko katika kitalu Na. F kiwanja Na. 13 katika mtaa wa Highland, ndani ya Jiji la Mbeya na ana nia ya kupangisha ghorofa ya pili katika jengo hilo.

**NA AMBAPO MPANGAJI** ni KAMPUNI YA UNUNUZI NA UZAJI WA DHAHABU yenye nia ya kupanga chumba kimoja katika ghorofa ya pili kwa matumizi ya ofisi pekee.

### **HIVYO BASI, PANDE ZOTE ZINAKUBALIANA YAFUATAYO:**

1. Mpangaji atachangia gharama za matumizi ambazo ni umeme, maji, ulinzi na usafi kwa kiasi kisichopungua shilingi laki moja na nusu (150,000/= kwa mwezi.
2. Kwamba mpangaji atahakikisha jengo hilo linatunzwa muda wote na kuwa katika hali nzuri.
3. Mpangaji hatafanya marekebisho ya kudumu katika jengo hilo bila ya kupata kibali cha maandishi toka kwa mpangishaji.
4. Kwamba pande zote mbili zitakaa na kufanya marejeo (*review*) pindi kutakapokuwa na haja ya kufanya hivyo.
5. Masharti ya mkataba huu yatabadilishwa kwa pande zote mbili kukaa pamoja na kufanya marejeo.

6. Kwamba upande wowote unaokusudia kuvunja mkataba huu utatoa notisi ya miezi sita kwa upande mwingine kabla ya kuvunjwa kwa mkataba.

**KWA KUSHUHUDIA MKATABA HUU PANDE HUSIKA ZINAWEKA SAINI  
KAMA IFUATAVYO:-**

IMESAINIWA NA Ailio Simoni  
M. Bwana KYN

AMBAYE NI AFISA MADINI MKAZI  
MKOA WA MBEYA leo tarehe 24 August 2023.

  
**MPANGISHAJI**


**MINING COMMISSION  
P.O. BOX 760  
MBEYA**

IMESAINIWA NA Zainali Maheboobali Asaria

MKURUGENZI WA KAMPUNI YA ELDORADO  
HOLDINGS TZ LTD

.....

MKOA WA MBEYA leo tarehe 24 August, 2023

  
**MPANGISHAJI**

  
ELDORADO HOLDINGS TANZANIA LIMITED  
P. O. Box 77244  
TIN: 168-128-441  
DAR ES SALAAM